MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA ARUSHA (ARUSHA WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-007

Mnamo Julai 2018 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Arusha (Arusha WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake kwa kipindi cha 2018/19 - 2020/21. Jedwali namba 1-4 yanaonesha mchanganuo wa bei na ada za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Matumizi kwa Uniti	Bei za Sasa		Bei zinazopendekezwa				
		2017/18	Mabadiliko Kwa %	2018/19	Mabadiliko Kwa %	2019/20	Mabadiliko Kwa %	2020/21
Majumbani	0 - 5	1030	20%	1236	12%	1,39	-10%	1,24
	>5 <15	1200	20%	1440	13%	1,620	-10%	1,455
	>15	1400	20%	1679	13%	1,89	-10%	1,69
Taasisi	0 - 5	1030	20%	1236	12%	1,39	-10%	1,24
	>5 <15	1120	20%	1344	13%	1,512	-10%	1,358
	>15	1200	20%	1440	13%	1,62	-10%	1,45
Biashara	0 -	1200	20%	1440	13%	1,62	-10%	1,45
	>5	1465	20%	1757	13%	1,97	-10%	1,77
	>11	1695	20%	2033	13%	2,28	-10%	2,05
Viwanda	0 - 5	1695	20%	2033	13%	2,28	-10%	2,05
	5 - 10	1850	20%	2219	13%	2,49	-10%	2,24
	> 10	2005	20%	2405	13%	2,70	-10%	2,43
Magati	Wote	780	20%	936	13%	1,05	-10%	945

Kundi la Wateja	Matumizi kwa Uniti	Bei za Sasa		Bei zinazopendekezwa				
		2017/18	Mabadiliko Kwa %	2018/19	Mabadiliko Kwa %	2019/20	Mabadiliko Kwa %	2020/21
Viwanda vya Kutengeneza Maji ya Chupa	Wote	11,830	20%	14,192	13%	15,969	-10%	14,339

Jedwali 2: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Uondoaji wa Maji Taka (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa		Bei zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadiliko Kwa %	2018/19	Mabadiliko Kwa %	2019/20	Mabadiliko Kwa %	2020/21
Majumbani	330	9%	360	8%	390	8%	420
Taasisi	450	11%	500	10%	550	9%	600
Biashara	660	8%	710	7%	760	7%	810
Viwanda	770	6%	820	6%	870	6%	920

Jedwali 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma – Shilingi/Kurejeshewa Huduma

Kundi la Wateja	Ada za Sasa		Ada Zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadiliko Kwa %	2018/19	Mabadiliko Kwa %	2019/20	Mabadiliko Kwa %	2020/21
Majumbani	15,000	7%	16,000	6%	17,000	6%	18,000
Taasisi	19,000	5%	20,000	5%	21,000	5%	22,000
Biashara	20,000	5%	21,000	5%	22,000	5%	23,000
Viwanda	26,000	4%	27,000	4%	28,000	4%	29,000

Jedwali 4: Gharama za Sasa na Zinazopendekezwa za Magari ya Kubebea Majisafi na Maji taka - Shilingi/Ukubwa wa Gari

Aina Ya Huduma	Gharama za Sasa	Gharama Zinazopendekezwa				
	2017/18	2018/19	Mabadiliko Kwa %	2019/20	Mabadiliko Kwa %	2020/21
Maji Uniti-10,000	-	106,000	6%	112,360	6%	119,102
Maji Uniti - 5000	-	84,80	6%	89,888	6%	95,281
Maji taka	-	84,80	6%	89,888	6%	95,281
Maji taka Uniti 5,000	-	68,90	6%	73,034	6%	77,416

Kutokana na maelezo ya Arusha WSSA, sababu kuu za kuomba mabadiliko ya bei ni: kupanda kwa gharama za pembejeo, kuchangia katika mradi wa kuboresha miundombinu ya majisafi na majitaka ya mji wa Arusha ambao unafadhiliwa pia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, kuongezeka kwa mahitaji ya watumishi kutokana na kuongezeka kwa eneo la kutoa huduma na kuanzisha ofisi katika kanda tano na matakwa ya kuboresha mishahara ya wafanyakazi ili kuvutia na kuendelea kuwa na wafanyakazi wenye sifa.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 20 Septemba 2018 katika Ukumbi wa Makumbusho – Azimio la Arusha** uliopo jiji la Arusha kuanzia saa **4:00 asubuhi.** Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Arusha WSSA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 25 Septemba 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA MAKAO MAKUU, GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA EWURA KANDA YA KASKAZINI - GHOROFA YA PILI, JENGO LA PPF PLAZA JIJINI ARUSHA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ARUSHA.**

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)
6 Septemba, 2018